## KISWAHILI : LUGHA

**Muda**: Saa 1 Dakika 40

***Chagua jibu lifaalo Zaidi kati ya yale uliyopewa kujaza mapengo.***

Harufu ya chawa ya maua, sauti __1__ ndege __2__ mkorogo __3___ sauti __4___ __5___ dirishani hadi chumbani __6__ Julia. ___7___ ya mijikaranda __8___ nje yalicheza na __9___ pambaja na ___10___. __11__ ukipiga na __12__ majani ___13___ kunoneana yakiuhongera upepo __14___. Julia, uso __15___ mashavu yaliyojaa ndu umechanuka, macho yameng"aa na tabasamu kuuvaa uso mzima.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. za | C. la | D. wa |
| 2. | A. kwa | B. katika | C. na | D. kwenye |
| 3. | A. wa | B. la | C. ya | D. za |
| 4. | A. lingine | B. jingine | C. wengine | D. nyingine |
| 5. | A. zilipenya | B. lilipenya | C. ulipenya | D. walipenya |
| 6. | A. alimokuwa | B. alichokuwa | C. alikokuwa | D. walimokuwa |
| 7. | A. mizizi | B. matawi | C. mimea | D. maganda |
| 8. | A. humu | B. huko | C. hapa | D. kwenye |
| 9. | A. kipiganisha | B. kupigania | C. kupigana | D. kupigishwa |
| 10. | A. mwangazo | B. kiangazi | C. pepo | D. upepo |
| 11. | A. uliokuwa | B. zilizokuwa | C. walizokuwa | D. yaliyokuwa |
| 12. | A. kuzifanya | B. Kulifanya | C. kuyafanya | D. kuzifanya |
| 13. | A. lenyewe | B. yenyewe | C. zenyewe | D. yenye |
| 14. | A. hayo | B. hilo | C. hizo | D. huo |
| 15. | A. wenye | B. zenye | C. lenye | D. yenye |

**Kutoka swai 16 mpaka 30 chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.**

16. Gani si nomino?
    A. uongo B. usafi
    C. wema D. sujudu
17. Vyakula **vizuri** vilipikwa na mama vizuri imetumika kama ___.
    A. kielezi B. kiarifa
    C. kisifa D. kivumishi
18. Ni sentensi gani imeandikwa katika kauli ya kutendewa?
    A. Alipigwa kwa sababu ya mchezo
    B. Shamba lililimwa vyema
    C. Mpira uliingiziwa pembezoni mwa kimia
    D. Salma alimkimbilia shangaziye
19. Nini maana ya nahau fanya inda?
    A. Kuwa mja mzito
    B. Fanya mtu asipate kitu
    C. Kuwa mjeuri
    D. Fanya kazi ya sulubu
20. Adili ni mtu mwadilifu, chauremb ni mtu mrembo ilhali Bakaya ni mtu mlafi. Majina kama haya ni _____.
    A. tashbihi B. majazi
    C. balagha D. jazanda
21. Andika wingi na ukanusho wa Waridi linapendeza
    A. Mawaridi hayapendezi
    B. Waridi halipendezi
    C. Lawaridi hayapendezi
    D. Nyaridi hazipendezi
22. Nini ukubwa na wingi wa sentensi ifuatayo?
    Kiti hiki kimevunjika
    A. majiti haya yamevunjika
    B. Majiviti hivi vimevunjika
    C. Majikiti haya yamevunjika
    D. Makiti hii zimevunjika
23. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika taarifa "Mkijibu maswali haya vyema, nitawatuza mwaka kesho," Mwalimu alisema.
    A. Mwalimu alisema kuwa tukijibu maswali hayo vizuri atatutuza mwaka ujao
    B. Mwalimu alisema kuwa tungejibu maswali hayo vizuri angetutuza mwaka ujao
    C. Mwalimu alisema kuwa tungejibu maswali yale vizuri atatutuza mwaka kesho
    D. Mwalimu alisema kuwa angetutuza baada ya mtihani mwako ujao

24. **Yeye** ni mtoto mweledi mno. Neno yeye limetumika kama.
   A. Kivumishi
   B. Kielezi
   C. Kiwakilishi
   D. Kiashiria
25. Andika kinyume cha Mfarika amenywea.
   A. Mfaniku amechachamaa
   B. Fahali amenenepa
   C. Mgumba amesinyaa
   D. Mbarika amenenepa
26. Askari wa kukodiwa huitwa _____.
   A. kachero B. mamluki
   C. mahuluki D. bawabu
27. Chagua neno ambalo ni kiunganishi katika sentensi hii. Mwalimu alienda darasani lakini hakufundisha.
   A. mwalimu
   B. alienda
   C. lakini
   D. darasani
28. Neno jingine lenye maana sawa na hamali ni ______.
   A. baradhuli
   B. mchoyo
   C. mdadisi
   D. mpagazi
29. Sehemu ya mwili inayosafisha damu ni ___.
   A. pafu B. figo
   C. kibofu D. ini
30. Neno uzalio liko katika ngeli gani?
   A. U-YA B. U-U
   C. I-ZI D. U-ZI

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 31-40**

Kefa Matendechere,
S.L.P 1212,
GAMEKAKA.
12/01/2016

Mwalimu wa Darasa la 8,
Shule ya Peponi,
S.L.P 90
GAMEKAKA.

Kwa Bibi,

**KUH : KUOMBA MSAMAHA KWA KUTOFANYA KAZI.**

Ninaandika barua hii ili kuomba msamaha kwa kutofanya kazi ya likizo ambayo ulitupa. Ninasikitika ya kwamba tulipofunga shule mwezi wa Disemba mwaka jana, niliambukizwa uwele wa mchochoto wa ubongo punde tu baada ya siku mbili za kufunga shule.

Awali, wavyele wangu walidhani ni homa ya malaria, hivyo basi wakaninunulia tembe za kumeza wakidhani ya kwamba ningepata afueni. Badala ya kupona, hali yangu ilizidi kuwa mbaya. Walipoona nikizidiwa, walinipeleka kwa tabibu na baada ya kupimwa, ikadhihirika dhahiri shahiri ya kwamba ni ukongo wa mchochoto wa ubongo !

Mara tu ilipogunduliwa hivyo, hatua za dharura zilichukuliwa za kunisafirisha kwa eropleni moja kwa moja hadi katika hospitali kuu ya „Aga Khan jijini Nairobi kule nililazwa mara moja. Waganga na waganguzi wakaanza pilkapilka zao za mchwa ili kuiokoa roho yangu. Haikuwa kazi rahisi, hata nusura wavyele wangu wakate tamaa kwani nilikuwa sijijui sijitambui si hayati si mamati. Nilikuwa nikichungulia kaburi.

Nililazwa hospitali humo kwa muda wa wiki nne. Hata hivyo, niliporuhusiwa kurudi nyumbani, nilikuwa bado nmedhoofika kisiha na kunyong‟onyea kiafya. Nisingeweza kamwe kuifanya kazi yoyote ya masomo maadamu tafakari zangu hazikuwa sawasawa.

Tafadhali ninaomba uniwie radhi kwa kutofanya kazi hiyo. Ninaahidi ya kwamba punde nitakapopata afueni nitaishughulikia kazi hiyo hatua kwa hatua hadi niikamilishe bila ajizi yoyote kwani ninafahamu kuwa ajizi ni nyumba ya njaa.

Ni matumaini yangu kwamba utaielewa hali yangu na kulikubali ombi langu.

Wako Mtiifu

Kefa Matendechere

31. Aina hii ya barua huitwaje?
    A. barua ya kidugu
    B. barua rasmi
    C. barua ya kuomba msamaha
    D. barua ya kirafiki
32. Aliyeandikuwa barua hii ni ______.
    A. mwalimu
    B. mwanafunzi
    C. kefa matendechere
    D. mwalimu wa darasa
33. Katika barua hii kusudi limeandikwa, yaani "kuomba msamaha kwa kutofanya kazi" sehemu hii huitwaje?
    A. kianzio  B. maamkizi
    C. mtajo  D. tamati
34. Ni sentensi gani si sahihi kulingana na taarifa?
    A. Mgonjwa anajali masomo yake
    B. Ugonjwa uliomwathiri mwandishi ni hatari
    C. Mwandishi hatawahi kuifanya kazi aliyopewa
    D. Mpokeaji wa barua hii yuko meru
35. Mwandishi anaomba msamaha hii ni ishara ya ____.
    A. utovu wa adabu
    B. uzembe kazini
    C. heshima
    D. uwongo
36. Homa ya malale huambukizwa na _____.
    A. mbu
    B. mbung"o
    C. mchochoto wa ubongo
    D. uwele
37. …..nilikuwa sijijui sijitambui….
    Hii ni tamathali gani ya lugha.
    A. Takriri  B. msemo
    C. tanakali ya sauti  D. semi
38. Neno kunyong"onyea limetumika katika taarifa. Maana yake ni _____.
    A. kuwa bora
    B. kuuma sana
    C. kudhoofu mwili
    D. kuwa na siha
39. Kamilisha methali kwa usahihi. AJizi ni ufunguo wa _____.
    A. njaa  B. umaskini
    C. heri  D. ajizi
40. Badala ya kuikamilisha barua hii kwa maneno "wako mtiifu." Pia mwandishi angeweza kuikamilisha kwa kuandika _____.
    A. Wako mpendwa
    B. Wako wa moyoni
    C. Wako wa dhati
    D. Wako mwaminifu

**<u>Soma ufahamu kisha ujibu maswali 41-50</u>**

Katika maisha ya binadamu hakuna sababy ya kukata tamaa.Ni heri kujikaza kisabuni hadi siku ya mwisho. Japo juhudi si pato, huenda tukafaulu mwishowe kwani papo kwa papo Kamba hulikata jiwe.

Zawadi alizaliwa katika familia fakiri kila mtu alikuwa mchochole, asiye na mbele wala nyuma. Zawadi alitupwa na mama yake mzazi siku chache baada ya kuzaliwa. Mambo hayo alifahamishwa alipokuwa na miaka thenashara. Kwa sababu alikuwa akiuliza kila siku walikokuwa wazazi wake. Jitimai isiyokuwa na kifani ilijaa katika moyo wake hakuelewa kwa nini hakuelezwa mambo yale. Aliamini kuwa dunia huzaa njema na vimbi, vikija vyema tushangilie na vikija vimbi tuvivumilie. Hakuwa na budi kuvumilia kwani lisilo na budi hubidi.

Ukweli wa mambo ni kuwa zawadi alizaliwa nje ya ndoa. Baba yake alikataa jukumu la uzazi naye mama yake kwa kushindwa kuelewa hatua ya kuchukua, akaamua kumtelekeza. Hapa ndipo alipookotwa na wasamaria wema waliompeleka katika nyumba ya mayatima. Akawa yatima aliyena wazazi wote wawili. Uchungu ulioje.Inaonekana kuwa mama yake aliamini kuwa mkono mmoja haumlei mwana.

Zawadi aliingiwa na hamu ya kuwaona wazazi wake. Alishindwa kumakinika shuleni kwani kila wakati alikuwa na mawazo belele yakimzunguka akilini kama pia. Aliamua kuanza harakati za kuwatafuta wazazi wake. Kazi hiyo haikuwa rahisi na mwishowe alirudi pale pale.

Katika nyumba za mayatuma baada ya kukata tamaa ama kweli mwenda tezi omo marejeo ni ngamani. Wafadhili wake walimpa moyo kuendelea na maisha yake ya kawaida. Alifanya hivyo na baada ya miaka mingi alihitimu kama daktari na kwenda kufanya kazi katika hospitali ya kitaifa. Aliwahudumia wagonjwa wengi kwa moyo wake wote. Zawadi alijaliwa kupata mchumba na baada ya miaka miwili wakafunga nikahi. Alijaliwa kuwapata watoto watatu, wawili wa kike na mmoja wa kiume.

Siku moja zawadi alikuwa akimhudumia mama mmoja hospitalini. Mama huyo alikuwa na mvuto wa ajabu kwa zawadi. Alimwonea huruma na kutaka kujua mengi. Mama yule akaamua kumweleza kila kitu bila kuficha chochote.

"Mwanangu najua mama yako anakuonea fahari sana. Bila shaka ni mama mwenye furaha. Mimi sina bahati.Nilipokuwa msichana, nilipata mimba kabla sijaolewa.Kijana aliyeniringia mimba akakataa katakata kunioa wala kunisaidia katika malezi ya mtoto yule.

Niliamua kumwacha njiani na kutoroka. Sijui kama alikufa au alipata msamaria mwema. Nilienda kuishi mji wa mbali ili nisijulikane. Baada ya muda mfupi nilimpata mchumba na akaniona lakini sikuweza kupata mtoto tena. Naamini Mungu alikifunga kizazi changukwa dhambi niliyotenda.

Zawadi aliduwaa. Akataka kujua Zaidi huku akijisemea moyoni, "Kumbe kuna wengi wanaofanyiwa kama mimi." Alimwuliza ni wapi alipomtupa mtoto wake na ni mwaka gani. Baada ya maelezo ya yule mama, Zawadi aliangua kilio kilichowashangaza wagonjwa wauguzi na jamaa za wa wagonjwa.

"Ni mimi mama uliyenitupa. Nimekulia katika nyumba ya mayatima ilhali nina wazazi!" Huzuni ilitanda. Vilio vya mama na bintiye. Huzuni, majuto na furaha vyote vilichanganyika. Daktari mkuu aliwachukua na kuwapeleka katika chumba maalum ili wapate fursa ya kuongea na wasiwasumbue wagonjwa wengine.

41. Methali "papo kwa papo Kamba hulikata jiwe" inamaana gani?
    A. Jambo lililo gumu likifanyiwa bidi mfululizo litawezekana
    B. Kujitahidi katika jambo Fulani si thibitisho la ufanisi
    C. Kufaulu kwa jambo lolote hakutegemei bidii
    D. Siri ya fanaka ni ulegevu
42. Zawadi alijua ukweli kuhusu wazazi wake alipokuwa na umri wa
    A. Miezi michache
    B. Miaka sita
    C. Miaka sita
    D. Miaka kumi na miwili
43. Ukweli wa mambo ni kuwa zawadi alikuwa _____.
    A. yatima
    B. mwanaharamu
    C. kiokote
    D. zumbukuku
44. Kwa nini Zawadi alikuwa akiuliza kuhusu wazazi wake.
    A. Alikuwa ameambiwa kuwa walikuwa hai
    B. Alijua walikuwa mahali Fulani
    C. Alitaka kujua kama walikuwa hai au walikufa ila awe na ukweli
    D. Alikuwa akiteswa katika nyumba ya mayatima na wahudumu kule
45. Matokeo ya kuwatafuta wazazi wake yaliishia vipi?
    A. Aliwatafuta mpaka akawapata
    B. Yalikuwa ya kuvunja moyo kwani hakufanikiwa
    C. Yalikuwa ya kutia moyo kwa sababu alipata fununu
    D. Alimpata baba yake lakini hakumpata mama yake
46. Kwa nini zawadi anaitwa yatima aliye na wazazi?
    A. Alikuwa na wazazi lakini hawakujulikana
    B. Wazazi wake walikufa akiwa mdogo
    C. Alikuwa na wazazi walezi lakini wazazi wake halisi walikuwa wamekufa
    D. Hakuwa na uhakika kuwa wazazi wake walikuwa hai
47. Kiokote ni nani?
    A. Mtoto aliyeokotwa
    B. Mtoto ambaye hana wazazi
    C. Mtoto anayeokota vitu mapipani
    D. Mtoto aliye na wazazi lakini wamemtelekeza
48. Mama yake zawadi alikuwa na jumla ya watoto wangapi?
    A. watatu B. wawili
    C. mmoja D. hatukuambiwa
49. Zawadi alikutana na mama yake wapi?
    A. zahanatini B. njiani
    C. kanisani D. hospitalini
50. Mama yake zawadi ana Imani gani kwa kutopata mtoto.
    A. Hakuhitaji mtoto mwengine
    B. Anaadhibiwa kwa dhambi aliyoitenda na kumtupa mtoto wake
    C. Mume wake alikuwa gumba
    D. Yeye mwenyewe alikuwa tasa